

Mchango wa Uhakiki-Maeneo katika Ufasiri wa Ploti katika Hadithi Fupi ya Kiswahili

*Shitemi J. M., Olali T., Mbutia E. M., & Wanjala, A.
Chuo Kikuu cha Nairobi*

Ikisiri

Utafiti wetu umejikita katika kuhusisha ufasiri wa ploti katika hadithi fupi ya Kiswahili na maeneo ya kijiografia kama yalivyosawiriwa katika hadithi fupi zenyewe. Nadharia mwafaka inayoshughulikia maeneo ya kijiografia katika kazi za kibunilizi ni uhakiki-maeneo. Kupitia usampuli maksudi tuliteua hadithi ya “Ahadi ya Mwana” ya Aidah Mutenyo kutoka diwani ya *Safari ya Matarajio na hadithi Nyingine*. Matokeo ya uchunguzi wetu yamedhibitisha kuwa uhakiki-maeneo wa maeneo ya kijiografia katika hadithi fupi ya Kiswahili, una manufaa makubwa kwa msomaji wa hadithi fupi ya Kiswahili kwa kuwa ubanifu wa maelezo kuhusu maeneo yenyewe huenda ukasababisha hadithi fupi kutofasirika kwa wepesi na haraka.

Maneno Muhimu: *Uhakiki-Maeneo, Mwanda, Homotopiki, Heterotopiki, na Tranto*

Utangulizi

Wahakiki wa utanzu wa hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili wamejizatiti kudadavua nduni za hadithi fupi. Baadhi yao (Mohochi 1995, Mwakio 2006, Nyutu 2016, Njeri 2018 na Makena 2018), walichunguza muundo wa hadithi fupi wakitumia nadharia ya umuundo. Ilhali wengine Makena 2018, ametumia nadharia ya kisosholojia kuchunguza maudhui. Utafiti huu, ni tofauti kutokana na uchunguzi huo wa awali kwa kuwa tumetumia nadharia ya uhakiki-maeneo kama ilivyoasisiwa na Westphal na kuenelezewa na washiriki wake. Nadharia hii inachangia kufafanua maeneo ambamo hadithi zimekitwa kisimulizi. tumetumia muhimili huu kufasiria ploti ya hadithi fupi ya Kiswahili. Huu ni mchango mkubwa katika uelewekaji wa hadithi fupi, licha ya kuwa, sifa ya ufupi wa utanzu wenyewe. Ufupi huu, unapelekea dondoti nyingi ambazo huenda zikawa kikwazo kwa msomaji kupata thamani za kifasihi kutoka hadithi husika.

Mapitio ya Maandishi

Wahakiki wengi wametoa vijelezi vingi kuhusu hadithi fupi. Baadhi ya vijelezi hivi ni, kuwa hadithi fupi, Mbatiah (2000: x) ameeleza hadithi fupi kuwa, ni masimulizi yaliyoandikwa katika lugha nathari kuhusu tajriba fulani ya maisha. Nao Timmammy na Swaleh (2013) wameeleza kuwa hadithi fupi,

...ina sifa za matumizi ya lugha ya nathari, masimulizi mafupi aghalab
ya tukio moja, mhusika mkuu mmoja au wahusika wachache, msuko
sahili na hatimaye mshikamano na umoja wa mawazo na mtindo.

Katika utafitu wetu, tutaeleza kuwa hadithi fupi ni: usimulizi mfupi wa kinathari ambao unaakisi tajriba fulani katika jamii. Hadithi fupi ni utanzu ambao umekua kwa kasi katika fasihi ya Kiswahili. (Timammy na Swaleh 2013:2). Ukuaji huu wa kasi ni sharti uambatane na uhakiki wa kazi zenyewe. Utafiti huu una azma ya kushughulikia mojawapo wa vipengele vya hadithi fupi-ploti. Vipengele vya hadithi fupi ni wahusika na uhusika, usimulizi, mtindo, ploti na maudhui kwa mujibu wa Jacobs (1993:51-59). Mhakiki Mbatiah (2000: xiv-xvi) anaona kuwa, dhamira, maudhui, mtindo, muundo na wahusika, ndivyo vipengele mojawapo muhimu cha hadithi fupi. Tunakubaliana na mawazo Jacobs kuwa ploti ni kipengele muhimu katika hadithi fupi. Kwa kuwa hakijataifitiwa ili kubaini umuhimu wake katika hadithi fupi ya Kiswahili. Utafitu wetu unajikita katika kujaliza pengo hili.

Ploti imeelezwa na wahakiki wengi. Mathalan, Jacobs na Roberts (1993:89) wanadai kuwa ploti hujengwa kwa mfuatano wa usababishi wa matukio katika hadithi. Huku Crane (1952) akieleza kuwa, ploti ni vitushi ambavyo viko kwenye hadithi, ambavyo kwavyo, matukio kutoka mwanzo, katikati

huchangia kuleta suluhisho mwishoni mwa hadithi. Naye Egan (1978:1) anaeleza ploti kuwa, ni usababishi amabao huleta muungano ambao huvyaza ukamilifu kutokana na utukiaji katika ulimwengu usio na mwisho. Kuwa, ploti ni hatima ambayo vipengele vyote vinapaswa kutimiza: ndio uhai wa kazi ya kifasihi. Egan anaendelea kueleza kuwa, ploti hurejelea muundo ndani wa hadithi ambao mawazo ya msomaji hudadavua. Kwa hivyo, anaona kuwa, ploti ni zao la uwazaji. Upande wake Johnson (1989:1) ameeleza kuwa bila ploti kazi za kubunilizi zitasambaratika katika vipengele vidogo vidogo. Hivyi kusababisha kutoweka kwa bunilizi hiyo. Neumeyer (1975: 5-18) ameeleza ploti kama matukio ya hadithi amabyo yamepangwa kisanii ambayo yamedhamiria kufurahisha na kuleta maana fulani. Anaongezea kuwa, ploti ni dhana ya kimsingi katika hadithi fupi. Yaani, ploti hushajiisha msomaji kuendelea kuisoma hadithi fupi. Kutokana na mapitio haya, tumedadavua kuwa kuwa ploti ni zao la mawazo ambalo hujengwa usababishi wa matukio hadithini. Huonyesha namana ambazo hadithi husonga mbele kutoa mwanzo hadi mwisho. Ploti sharti ipangwe kisanii ili kuibua maana inayotazamiwa.

Utafiti wetu umejikita katika dhana ya usawiri wa maeneo ya kijiografia katika hadithi fupi na jinsi ambazo usawiri huu unaauni ufasiri wa hadithi hizo kwa kuzingatia kipengele cha ploti. Mbinu mwafaka ya kutusaidia kueleza uhusiano huu ni uhakiki-maeneo. Nadharia hii iliasisiwa na Bertrand Westphal. Pamoja na wenzake Kama Prieto (2011, 2012) na Tally (2013) wamedhihirisha ufaafu wa uhakiki-maeneo katika kuchambua maeneo ya kijiografia katika hadithi za kubunilizi. Westphal (2011:2) alieleza kuwa, uhakiki-maeneo utatupelekea kusesitiza njia ambazo fasihi inatagusana na ulimwengu halisi. Kuwa, uhakiki-maeneo utatusaidia kufahamu maeneo halisi kupitia kufahamu maeneo hayo kupitia fasihi. Smethurst (2014:1) amefafanua uhakiki-maeneo kama mtazamo wa kuchunguza maeneo katika matini za kifasihi. Naye, Mannolini (2023:5) ameeleza kuwa uhakiki-maeneo unatusaidia kuhusisha mwanda maeneo, tuliotagusana nao au wa kufikirika ili tupate mkabalawa mwandishi wa kazi za kubunilizi.

Hivyo, uhakiki- maeneo unahusisha zoezi la kuhakiki kazi za kubunilizi kwa kuzihusisha na maeneo yake katika ulimwengu halisi. Uwasilishaji wa maeneo katika bunilizi yakihusishwa na maeneo katika ulimwengu halisi huvyaza aina tatu za uwasilishaji. Uwasilishaji wa maeneo katika hadithi kama tunavyoyafahamu (homotopiki); uwasilishaji wa maeneo tofauti kama tunavyojua katikaulimwengu halisi (heterotopiki) na uwasilishaji wa kubunifu kama katika maandishi ya kinjozi (tranto).

Wanauhakiki-maeneo huzingatia vipengele vifuatavyo katika katika shughuli yao: huzingatia maeneo ya kijiografia katika bunilizi; dhana ya urejelezi na kuhusisha maneneo ya kijiografia katika hadithi na ulimwengu halisi. Aidha, huhusisha mwanda-wakati (spatiotemporality); matumizi ya fahiwa ainati; mpangilio-safu; mwingiliano wa matini kama sehemu ya dhana ya urejelezi na mtazamo-kwingi, Westphal (2011:3).

Westphal (2011:3) anasisitiza kuwa, kazi za kibunilizi zinaweza kutegemewa kama nyenzo nyinginezo za kuelewa ulimwengu. Kwa sababu, uhakiki-maeneo ni zoezi la kihakiki ambalo wasomaji hujihusisha na mwanda wa maeneo ambao hujenga maisha kupitia tajriba za wanajamii za maisha kadhalika kupitia taswira zinazotarajiwa kikamilifu. Ufaafu huu wa uhakiki-maeneo ndio ulitupelekea kuteua kuchunguza mchango wake katika ufasiri wa ploti katika hadithi fupi ya Kiswahili.

Mbinu za Kukusanyia Data

Utafiti huu ni wa maktbani. Tulisoma, kuchambua matini kuhusu nadharia ya uhakiki-maeneo, hadithi fupi na ploti. Aidha, tulisoma hadithi fupi. Tukitumia sampuli makusudi tuliteua hadithi ya “Ahadi ya Mwana” ya Aidah Mutenyo kutoka diwani ya Safari ya *Matarajio na Hadithi nyingine*. Hadithi hii tuliiteua kwa kuwa, ilikuwa na maeneo ya kijiografia dhahiri na ploti angavu. Hadithi hii ilitupa nafasiya kutagusana na maeneo mengi ya kijiografia ambayo yalituptia fursa ya kuyahusisha hayo na ukuzaji wa ploti wa hadithi ya “Ahadi ya Mwana”.

Matokeo ya Uchunguzi

Hadithi ya “Ahadi ya Mwana” inahusisha maeneo yafatayo ya: shuleni anakosomea Anaseti, kuna maeneo mbalimbali kama vile uwanjani na afisi ya Mwalimu mkuu; nyumbani kwa mzee Gonza ambako matukio kadhaa yanatukia; sokoni; hosipitalini; kanisani mara mbili; kituo cha biashara cha Nchanga; nyumbani kwa askari na kituo cha polisi. Matukio katika maeneo haya yanashajiisha ploti ya hadithi. Tutachunguza misukumo katika maeneo haya ambayo yanasabibisha wahusika kuchukua hatua fulanifulani ambazo zinaleta athari ya kipekee katika usukaji wa hadithi yenyewe.

Nguli wa hadithi ya “Ahadi ya Mwana” ni Anaseti mwanafunzi katika shule ya Upili ya Bunyangabo. Hadithi inaanzia katika shule hii ya Bunyangabo. Anaseti anakataa kula na wenziwe wakati wa chamcha. Anaseti anaona haya, Mukisa rafiki alimrai wale pamoja lakini alikataa. Anaseti alimwambia kuwa, “Si ati sitaki kula pamoja nanyi, ila aona aibu. Kila mara nyinyi hubeba vyakula vya aina mbalimbali. Mimi wakati wote hubeba muhogo huo huo.” Licha ya Mukisa kumsaili na kumtuliza Anaseti, mwandishi anatueleza kuwa, “Maneno ya Mukisa kila mara yalizua mjadala mkubwa akilini mwa Anaseti,” (uk 109). Matukio katika eneo hili la shule, yanafanya Anaseti kuona muhogo kama adhabu kwake, (uk 109). Japo Muhogo ulikuwa na thamani za kiafya, dadake wa kambo hakuubeba shuleni kama alivyofanya Anaseti. Anaseti anachukua hatua ya kutoula muhogo shuleni.

Alipofika nyumbani kwao, Anaseti alikula muhogo wake na kuuteremsha na maji. Wakati huo huo alitokwa na machozi. Alilia kwa kite huku akilaani jaala ambayo ilimleta katika familia ile. Alilaani sana kifo cha mamake mzazi.

Ni wakati huu ndipo kupitia mbinu rejeshi mwandishi wa hadithi ya “Ahadi ya Mwana,” anatumia kadhaa ya Anaseti. Anaseti ni mwanawe mzee Gonza na mkewe marehemu Nakalanzi. Mamake Anaseti aliaga dunia wakati akijifungua huyohuyo Anaseti. Walipotoka nyumbani kwenda hosipitali mzee Gonza na mkewe kwa baisikeli ya mzee Gonza, walikuwa na matumaini ya kurejea salama nyumbani. Huko hosipitalini mambo yaliharibika. Kwa sababu ya *pressure* mama mtoto hakutoka salama. Hosipitali ambayo ilitarajiwa kuwa mahali pa afueni kwa familia hii, kukawamahali pa majonzi na jitimai. Ujane huo ulimpelekea mzee Gonza kumlea mwanawe akiwa pweke. Katika miaka ya awali ya Anaseti katika shule ya msingi.

Baada ya mwongo mmoja, akiwa nyumbani kwake mzee Gonza alipata hamu ya kuoa. Kupitia mawazo yam zee Gonza, mwandishi anasema kuwa, “... ujane una makeke...naona kwamba ninashitaji mtu wa kunisaidia malezi...,” (uk 112). Baada ya mawazo haya ambayo yalijitokeza kupitia sala kwa marehemu mkewe, mzee Gonza alianza kutafuta mke, (uk 112).

Mzee Gonza alibahatika kumpata mke katika soko la kwao. Kwa hakika alikuwa mshitiri wa yule mwanamke. Walifunga ndoa katika kanisa alikofungia ndoa na marehemu mkewe. Eneo hilo la kanisani, halikumpa bashasha kama mwanzo. Japo alijitia moyo kuwa ndoa yake ingefaulu.

Nakato mke wa mzee Gonza alipata kifungusa mimba, mtoto wa kike. Nakato hakuwa na furaha kupata kifungua mimba wa kike. Alihisi kuwa jamii ya mumewe haitamthamini. Mwandishi anatueleza kuwa, “...alihofia kuwa mume wake angempenda zaidi Anaseti, (uk 113). Anaseti alipoingia katika shule ya sekondari, mamake wa kambo hakumthamini. Alimtesa hata Anaseti hakupata nafasi ya kufanya kzai zake za shuke bali alipewa majukumu ya nyumbani. Mwandishi anatueleza kuwa, “Baadhi ya siku Anaseti hakuhudhuria masomo,” lakini “...alivumilia hali hiyo na kula yamini kutia bidii masomoni,” (uk 113). Kadhalika, Anaseti alikosa mahitaji muhimu maishani. Japo mzee Gonza alimtumia mkewe masurufu ya kutosha. Mkewe alikuwa mchoyo kwa anaseti. Alimghilibu mumewe kila alipopiga simu kuwa Anaseti alikuwa akiendelea vyema masomoni. Eneo hili la kwao pamoja na kupewa muhogo kila siku, yalimpelekea Anaseti kupanga kutoroka nyumbani kwao.

Safari ya utoro ya Anaseti ya kuelekea mjini Jinja, ilimfikisha usiku katika kituo cha biashara cha Nchanga. Hapa kundi la vijana wa mtaani lilimsuta Anaseti, kumbughudhi na kumfanyia makuruhi. Alipata shufaa wakati askari wa kike alipotokea. Wale vijana wakatoweka. Baada ya kumsaili Anasetina kuelewa shida yake, askari huyo alimpeleka Anaseti kwake. Mume wa askari huyo

na mkewe walimpeleka Anaseti kwa mkuu wa Kituo chao cha polisi. Mkuu huyo, alimpigia Mwalimu mkuu wa shule ya anaseti simu.

Keshoye, Anaseti alipelekwa na karandiga ya polisi shuleni. Askari wakamweleza Mwalimu wake mkuu mateso ya anaseti nyumbani kwao. Mwalimu mkuu alimwita Nakato. Mwandishi anaeleza kuwa, "... alijutia makosa yake", kisha aliomba aende na Anaseti. Mwalimu mkuu alimhimiza Anaseti aendelee kuwa mtiifu kwa mamake. Japo Anaseti alikubali kurudi nyumbani, alirudi shinda upande, hakuamini toba ya nakato. Alidhamiria kutia bii masomoni ilia pate afueni ya kwenda kusomea mbali na kwao.

Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalipotangzwa, Anaseti aibuka kuwa mwanafunzi bora shuleni kwao na nchini. Dadake wa kambo alimhongera. Anaseti alimtia moyo pia naye angefaulu katika masomo yake akifanya bidi. Mzee Gonza alipofika nyumbani, mkewe alimpa gazeti ambalo lilikuwa na taarifa za ushindi wa Anaseti. Babake na dadake Anaseti walifurahia huku mamake a kambo, "Alikuwa amejawa na aibu na majuto, moyo wake ukimuhukumu," (uk 115). Haya yote yakiendelea, Anaseti alikuwa amesimama mlangoni, huku akimtazama Nakato. "Kwa mara ya kwanza Anaseti aliona imani na furaha ya dhati kwenye uso na macho ya Nakato. Jambo hili lilimfanya Anaseti kutamani kuwa mamake mzazi angalikuwako hapo katika furaha hiyo. Kimoyomoyo alimtungia shairi la kumhongera.

Matukio katika kiambo cha mzee Gonza, shuleni, kituo cha biashara na polisi, afisini kwa Mwalimu mkuu yanakuwa muhimili mkuu ambako ploti ya hadithi ya "Ahadi ya Mwana" inajengeka. Matukio katika maeneo hay yanashajiisha na kudhibiti ploti ya hadithi ya "Ahadi ya Mwana." Hivyo kudhihirisha kuwa, usawiri wa maeneo ya kijiografia katika hadithi fupi ya Kiswahili unasaidia ufasiriwa ploti pamoja na vipengele vingine vya hadithi fupi.

Hitimisho

Kutokana mjadala wa Makala hii ni bayana ya kwamba kipengele cha msuko katika kazi za kubuni na hasa katika hadithi fupi kinapaswa pia kuchambuliwa kwa kutumia mikakakti mipya ambayo inaibua mambo ambayo yanaweza kuachwa kama yanaelea. Umihimu wa kukita mtazamo huu katika utanzu wa hadithi fupi ni kutokana na ukweli ya kwamba utanzu huu huwa umebanwa kimaelezo katika maeneo ya maudhui na fani. Hii ina maana ya kwamba maswala mengine hayabainiki moja kwa moja. Hii ni tofauti na riwaya ambayo huabiri masafa marefu na kumpatia mwandishi nafasi ya kukuza maudhui na fani kwa kutegemea mapenzi yake na ubunifu wake.

Hadithi fupi za Kiswahili zilizo na ploti dhahiri ambazo zina maeneo ya kijiografia zina uwezekano wa kufasirika kwa kina hivyo kueleweka kwa wepesi. Maeneo ya kijiografia katika hadithi fupi yanaibua maana katika hadithi husika hata kama maeneo yenyewe hayataelezwa kwa undani sana. Sifa ya ubunifu wa maelezo unatatuliwa pakubwa na usawiri wa maeneo ya kijiografia kikamilifu.

Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa utafiti kuhusu athari za maeneo ya kijiografia kwa wahusika katika hadithi fupi utekelezwe ili kubaini mwingiliano wa maeneo ya kijiografia hadithini na wahusika. Aidha, uteuzi wa toni ya hadithi fupi ihusishwe na maeneo ya kijiografia ili kubaini uteuzi wa lugha katika maeneo mabimbali katika hadithi fupi ya Kiswahili. Mapendekezo haya yakitekelezwa uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili utakuwa umeongezewa makali na kusongezwa mbele katika masafa ya ukuaji. Kwa upande mwingine wasomaji wa tahakiki wa kazi zilizoandikwa kwa mikakati hii watakuwa wamepewa fursa ya kufasiriwa mambo mengi ambayo aghalabu yanguwapita.

Marejeleo

- Crane R. S (1952). The concept of Plot and the Plot of Tom Jones. *The Novel: anthology of Criticism and theory*. Chicago University Press: Chicago.
- Crowley D. (2011). Introduction: charting a Path for Geocriticism. Katika: *Africa's Narrative Geographies. Geocriticism and Spatial Literary Studies*. Palgrave Macmillan. New York.
- Egan K. (1978). What is Plot? *New Literary History, Vol. 9. /No 3, Rhetoric I: Rhetoric Analysis*. PP 435-473.
- Johnson D. (1989). The Importance of Plot. *The Three-Penny Review. No. 36*. PP 13-15.

- Makena E. M (2018). *Uwasilishaji wa Maudhui katika Hadithi Fupi Tenle za Said A. Mohammed*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijchapishwa.
- Mbatiah A. (2000) (Mh). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Jomo Kenyatta foundation: Nairobi.
- Mbuthia E. na Matei K. A (Wh), (2022). *Safari ya Matarajio na Hadithi Nyingine*. Spotlight Publishers Limited: Nairobi.
- Mwakio W. L (2006). *Matumizi ya Tashibibi, Sitiari na Taashira katika Divani ya Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijchapishwa.